Matarajio ya ukuaji wa watoto

80% ya ukuaji wa ubongo wa binadamu unafanyika katika miaka mitatu ya mwanzo wa maisha yake!

Watalaam wa matibabu ya watoto pamoja na Kituo cha Kudhibiti Ugonjwa Marekani wameonesha wazi kiwango cha kukomaa kwa ubongo wa watoto kwa kila umri, hadi umri wa mezi 12.
Kiwango cha ukuaji kinaonekana kwa vitu watoto wengi wanaweza kufanya kwa umri fulani.Ni kitu muhimu kutizama kiwango cha ukuaji kwa tahadhari; kwa sababu kila mtoto ana namna yake ya kukomaa. Kuna watoto wanawokomaa kwa kawaida bila kuwa na alama teule ya kiwango chaa umri wake. Wazazi wanaombwa kumualifu mganga wa watoto wawo iwapo wanaona ukuaji wa watoto wawo una matatizo au unacelewa.

Ni vitu gani mtoto wako anaweza kufanya kwa umri wake?

Lugha na maendeleo ya mawasiliyano

- Mtoto anajibu maombi sahihi ya sauti
- Anajua kutumia ishara sahihi ya kicwa, kama vile kumaanisha "hapana".
- Anabwabwaja akigeuza sauti
- Anajua kusema "dada" na "mama" pamoja na "oh-oh!"
- Anajaribu kutamka maneno ya kawaida au kusema fungu ya sentensi

Ukuaji wa kijamii/wa mhemuko

- Kulia akiona mzazi au mlezi anaondoka
- Anajihadari wageni wakiwepo
- Anaonesha kuwa na hofu akiona matokeo fulani
- Kuna vitu vya kuchezeya watoto avyopendelea kuliko vingine
- Anampenda sana mama mzazi au mlezi kuliko watu wenginele
- Anaweza kuwa anahofia matokeo fulani
- Anarudiarudia kunakili sauti na ishara ya mikono
- Anajilisha mwenyewe na mikono yake
- Anatangulia kusoma au kucheza kwa kukupatia kitabu au kitu cha kuchezea watoto
- Akivalishwa, anasaidia kwa kuleta mikono au miguu yake mwenyewe

Umri wa mezi 12

Shirika la watalaam wa matibabu ya watoto marekani linapendekeza watoto wote kutathminiwa kwa umri wa miaka :

- mezi 9
- mezi 18
- mezi 24 au 30

Vifaa vilivyopendekezwa vya kutahmini kukomaa kwa watoto :

- Hojaji ya umri na ulingo**(PEDS)**
- Tathmini ya wazazi kuhusu kukomaa kwa watoto**(PEDS-DM)**
- Tathmini ya Brigance

Recommended Apps:

GET IT ON Google Play

Download on the App Store

CDC's Milestone Tracker
Daily Vroom
BabySparks

Ofisi ya elimu ya msingi ya mashule ya serikali mjini Buffalo

MY BROTHER'S KEEPER MBK

Maelezo haya ametolewa na American Academy of Pediatrics at https://www.aap.org Vituo vishugulikavyo na kudhibiti ugonjwa Marekani kwa https://www.cdc.gov/ na aligharamiwa na My Brother's Keeper Initiative ya uongozi wa mashule.

Ukuaji wa tambuzi (kujifunza, kufikiria, akili ya kupata suluhu la tatizo)

- Anachunguza vitu kwa njia nyingi (kutikisa, kugogota, kutupa, kuangusha
- Kugunduwa vitu vilivyofichwa kwa urahisi
- Anaonesha kwa kidole anavyotaka
- Anageukia/anaonesha picha baada ya kusikia jina kamili likitajwa
- Anaiga wanavyofanya watu wengine
- Anaanza kutumia vilivyo vifaa vya kawaida (kunywa kwa kikombe,kucanua nywele, kusafisha meno, kuzungusha namba za simu)
- Anaweza kufuata mwongozo hatuwa kwa hatuwa (kuleta mpira, kuogota kitu)

Ukuaji wa viungo (gross motor)

- Anatambaa akitumia mikono na magoti kwa kutegemeza wuili wake
- Ana uwezo wa kujikalisha mwenyewe bila mtu yoyote kumsaidia
- Anajitahidi kusimama
- Anaweza kutembea akishika viti
- Anasimama na kubakia hivo hivo bila msada
- Anaweza kuenda hatua moja, mbili au tatu bila msada

Anakomaa kwa kuanza kutumika

- Anaweza kushika mikononi (kidole cha shahada na kidole gumba) hasa wakati anashika chakula
- Anagonganisha vitu viwili
- Anaweka vitu ndani na kuvitoa nje ya kopo/mkebe
- Anashika vitu mikononi na kuachiliya akitaka
- Anagusa/anaonesha akitumia kidole gumba
- Anajaribu kunakili mandishi

Nimuambie nini mganga wa mtoto wangu?

Kila mtoto anakomaa kwa namna yake pekee. Hautaweza kujua ni siku gani mtoto wako ataiga akili fulani. Ni vizuri kuwasiliyana na mganga wa mtoto, kama iwapo anaonesha ishara za ukuaji wake unachelewa.

- Kama hatambae
- Kama anatambaa kwa mikono bila kutumia magoti yake
- Kama hawezi kusimama hata akisaidiwa
- Kama hawezi kutafuta na kupata vitu vilivyofichwa akiangalia
- Kama hatowe sauti au haseme neno ("kama mama" au "dada" au "baba")
- Kama haige kutumia mikono yake kama kutikisa, kupeperusha au kutikisa kichwa
- kama hawezi kuonesha vitu au mapicha na kidole cha shahada
- Kama anasahau kufanya ishara alikua anafanya kwa ufundi

Namna mzazi anaweza kumsaidia mtoto wake kukomaa na kuiga

Ongea na mtoto wako bila kuchoka. Tumiya maneno anayoweza kumsaidia kuiga vitu vya kawaida. Mfano: "Mommy anatumia kichanuwa chako kwa kuchanua nywele zako."

Soma ukiwa na mtoto wako kila siku. Muache mtoto abadilishe ukarasa na badilishana naye kutaja mapicha aliyomomkwa litabu.

Jibu kama unasikia mtoto akitoa sauti au akipiga kelele. Itamsaidia kuiga maneno ya kuongea.

Muimbie wimbo mtoto wako. Na cheza nae.

Shika muda mrefu ukumkumbatiya mtoto wako.

Mpongeze mtoto wako na muoneshe kuwa unamhudumiya kwa upendo.

Mpe mtoto karatasi na karamu na mwache achore kama anavyopenda yeye.

Chez ana mtoto wako ukitumia vitu mbalimbali vya kuchezea watoto, umbo za kufanana/tofauti, na kadhalika.

Ficha vitu vya kuchezea watoto na mwache mtoto agunduwe mahali vilipo

MY BROTHER'S KEEPER MBK

Maelezo haya ametolewa na American Academy of Pediatrics at https://www.aap.org Vituo vishugulikavyo na kudhibiti ugonjwa Marekani kwa https://www.cdc.gov/ na aligharamiwa na My Brother's Keeper Initiative ya uongozi wa mashule.

Maelezo haya ametolewa na
American Academy of Pediatrics at https://www.aap.org Vituo vishugulikavyo na kudhibiti ugonjwa Marekani kwa https://www.cdc.gov/ na aligharamiwa na My Brother's Keeper Initiative ya uongozi wa mashule.